09

# OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA WANAWAKE NA WATOTO - ZANZIBAR SEPTEMBA MWAKA 2022

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 170 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Septemba,2022. Jumla ya waathirika 170 kati ya hao, waathirika Wanawake ni 18 (asilimia 10.6) na watoto ni 152 sawa na asilimia 89.4, miongoni mwao wasichana walikuwa 110 (asilimia 72.4) na wavulana walikuwa 42 (asilimia 27.6).


**Kielelezo 1.1 Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Septemba 2022**




**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Wilaya ya Mjini imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 47), ikifuatia Wilaya ya Magharibi "B" ambapo kumeripotiwa matukio 45. Wilaya ya Mkoani imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote ambapo matukio manne (4) yameripotiwa wakati Wilaya ya Micheweni hakukuripotiwa tukio lolote kwa mwezi wa Septemba 2022 .

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Septemba 2022**




**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi – Zanzibar**

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 29.8 kutoka matukio 131 kwa mwezi wa Agosti, 2022 hadi 170 mwezi wa Septemba, 2022. Aidha, Wilaya ya Magharibi"A" iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Agosti 2022 (matukio 31) na Wilaya ya Mjini imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Septemba 2022 (matukio 47). Wilaya ya Micheweni imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote (tukio moja (1)) kwa mwezi Agosti 2022.Wilaya ya Mkoani imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote (matukio manne (4)) na Wilaya ya Micheweni hakukuripotiwa tukio lolote kwa mwezi Septemba 2022.

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Agosti na Septemba 2022**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 |
| Kaskazini 'A' | 7 | 6 | 6 | 2 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 7 | 2 | 3 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 |
| Kati | 8 | 6 | 7 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 9 | 3 | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Mjini | 25 | 47 | 11 | 21 | 12 | 7 | 1 | 4 | 0 | 1 | 1 | 4 | 0 | 10 |
| Magharibi 'A' | 31 | 33 | 10 | 12 | 10 | 8 | 4 | 2 | 0 | 0 | 7 | 4 | 0 | 7 |
| Magharibi 'B' | 29 | 45 | 24 | 24 | 5 | 8 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 6 |
| Wete | 7 | 8 | 5 | 2 | 0 | 3 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 5 | 3 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 6 | 4 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **131** | **170** | **75** | **77** | **32** | **32** | **7** | **14** | **3** | **12** | **12** | **12** | **2** | **23** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 88.9 kutoka matukio 90 kwa mwezi wa Septemba, 2021 hadi 170 mwezi wa Septemba, 2022. Aidha, Wilaya ya Magharibi”B” iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Septemba 2021 (matukio 21) ambapo Wilaya ya Mjini imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Septemba 2022 (matukio 47).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Septemba 2021 na Septemba 2022**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 6 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 7 | 4 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 9 | 6 | 6 | 3 | 0 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 9 | 3 | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Mjini | 13 | 47 | 4 | 21 | 5 | 7 | 0 | 4 | 1 | 1 | 2 | 4 | 1 | 10 |
| Magharibi 'A' | 11 | 33 | 6 | 12 | 3 | 8 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 4 | 2 | 7 |
| Magharibi 'B' | 21 | 45 | 12 | 24 | 3 | 8 | 0 | 3 | 1 | 3 | 2 | 1 | 3 | 6 |
| Wete | 9 | 8 | 5 | 2 | 0 | 3 | 0 | 0 | 2 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 5 | 3 | 3 | 1 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 4 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **90** | **170** | **50** | **77** | **14** | **32** | **3** | **14** | **7** | **12** | **10** | **12** | **6** | **23** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Miongoni mwa watoto 152 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 70, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 32, wasichana walioingilia kinyume na maumbile ni 14, Kutorosha walikuwa ni watatu 11 wote ni wasichana, shambulio la aibu walikuwa tisa(9) ambapo wasichana walikuwa wanane (8) na mvulana mmoja (1) na shambulio walikuwa 16 ambapo wasichana walikuwa saba(7) na wavulana walikuwa tisa(9).

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Septemba 2022**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 6 | 2 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 6 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 9 | 4 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 41 | 19 | 7 | 4 | 1 | 0 | 3 | 0 | 3 | 4 |
| Magharibi 'A' | 27 | 10 | 8 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 3 |
| Magharibi 'B' | 40 | 22 | 8 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 |
| Wete | 8 | 2 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **152** | **70** | **32** | **14** | **11** | **0** | **8** | **1** | **7** | **9** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Miongoni mwa wanawake 18 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa saba (7) , kutorosha alikuwa mmoja(1), shambulio la aibu walikuwa wanawake watatu (3) na shambulio walikuwa wanawake saba (7).

**Jadweli 1.4: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya, Septemba 2022**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 6 | 2 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Magharibi 'A' | 6 | 2 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 5 | 2 | 0 | 1 | 0 | 2 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **18** | **7** | **0** | **1** | **3** | **7** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 58) sawa na asilimia 38.2 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 51) sawa na asilimia 33.6. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17(matukio 34) sawa na asilimia 48.6 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Septemba 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 4 | 3 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| 6-10 | | 8 | 15 | | | 6 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 1 | 36 |
| 11-14 | | 24 | 10 | | | 6 | 0 | 2 | 0 | 2 | 4 | 3 | 51 |
| 15-17 | | 34 | 4 | | | 2 | 0 | 9 | 1 | 0 | 5 | 3 | 58 |
| **Jumla** | | **70** | **32** | | | **14** | **0** | **11** | **1** | **8** | **9** | **7** | **152** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Septemba, 2022 yameongezeka kwa asilimia 27.7 (matukio 152) ukilinganisha na mwezi wa Agosti, 2022 (matukio 119). Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwezi uliopita imeongezeka kwa asilimia 5.5 kutoka matukio 55 kwa mwezi Agosti 2022 hadi matukio 58 kwa mwezi wa Septemba 2022.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Agosti na Septemba 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | Jumla |
| | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 |
| 0-5 | 1 | 4 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 7 |
| 6-10 | 6 | 8 | 6 | 15 | 3 | 6 | 0 | 0 | 3 | 6 | 0 | 1 | 18 | 36 |
| 11-14 | 20 | 24 | 17 | 10 | 3 | 6 | 0 | 2 | 3 | 2 | 0 | 7 | 43 | 51 |
| 15-17 | 42 | 34 | 7 | 4 | 1 | 2 | 3 | 9 | 2 | 1 | 0 | 8 | 55 | 58 |
| **Jumla** | **69** | **70** | **32** | **32** | **7** | **14** | **3** | **11** | **8** | **9** | **0** | **16** | **119** | **152** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwa mwaka uliopita imeongezeka kwa asilimia 87.7 kutoka matukio 81 kwa mwezi wa Septemba, 2021 hadi matukio 152 kwa mwezi wa Septemba, 2022, ambapo idadi ya matukio katika umri wa miaka yote yameongezeka kwa mwezi wa Septemba 2022.


**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Septemba 2021 na Septemba 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Sept 2021 | Jumla Sept 2022 |
| | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | | |
| 0-5 | 0 | 4 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| 6-10 | 3 | 8 | 4 | 15 | 1 | 6 | 0 | 0 | 4 | 6 | 0 | 1 | 12 | 36 |
| 11-14 | 13 | 24 | 7 | 10 | 1 | 6 | 0 | 2 | 5 | 2 | 0 | 7 | 26 | 51 |
| 15-17 | 28 | 34 | 3 | 4 | 1 | 2 | 6 | 9 | 0 | 1 | 5 | 8 | 43 | 58 |
| **Jumla** | **44** | **70** | **14** | **32** | **3** | **14** | **6** | **11** | **9** | **9** | **5** | **16** | **81** | **152** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Matukio 138 kati ya matukio 170 yametokea nyumbani sawa na asilimia 81.2 na matukio 32 yametokea sehemu nyengine sawa na asilimia 18.8.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea, Septemba 2022**




**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Mlinganisho wa matukio yaliyotokezea nyumbani kwa mwezi yameongezeka kutoka matukio 58 kwa mwezi wa Agosti, 2022 hadi matukio 138 kwa mwezi wa Septemba, 2022. Aidha, matukio yaliyotokea sehemu nyengine yameonyesha kupungua kwa asilimia 56.2 kutoka matukio 73 hadi matukio 32 kwa miezi hiyo.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Maeneo yaliyofanyika Matukio, Agosti na Septemba 2022**

| Eneo la Matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | Jumla Sept 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | |
| Nyumbani | 40 | 65 | 6 | 29 | 1 | 6 | 1 | 9 | 8 | 6 | 2 | 23 | 58 | 138 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 35 | 12 | 26 | 3 | 6 | 8 | 2 | 3 | 4 | 6 | 0 | 0 | 73 | 32 |
| **Jumla** | **75** | **77** | **32** | **32** | **7** | **14** | **3** | **12** | **12** | **12** | **2** | **23** | **131** | **170** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Mlinganisho wa idadi ya matukio yaliyotokea nyumbani kwa mwaka yameongezeka kutoka matukio 61 kwa mwezi wa Septemba 2021 hadi matukio 138 kwa mwezi wa Septemba 2022. Aidha idadi ya matukio yaliyotokea sehemu nyengine yameongezeka kwa asilimia 14.3 kutoka matukio 28 kwa mwezi wa Septemba, 2021 hadi 32 mwezi wa Septemba, 2022.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Septemba 2021 na Septemba 2022**

| Eneo la Matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Sept 2021 | Jumla Sept 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | | |
| Nyumbani | 33 | 65 | 13 | 29 | 1 | 6 | 3 | 9 | 5 | 6 | 6 | 23 | 61 | 138 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Sehemu nyengine | 16 | 12 | 1 | 3 | 2 | 8 | 4 | 3 | 5 | 6 | 0 | 0 | 28 | 32 |
| **Jumla** | **50** | **77** | **14** | **32** | **3** | **14** | **7** | **12** | **10** | **12** | **6** | **23** | **90** | **170** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Matukio 125 kati ya matukio 170 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Polisi sawa na asilimia 73.5, matukio 39 yapo Ofisi ya Mashtaka sawa na asilimia 22.9 na matukio sita(6) yapo mahakamani sawa na asilimia 3.5.


**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa, Septemba 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 77 | 7 | 70 | | 3 | 0 | 0 | 0 | 24 | 50 |
| Kulawiti | 32 | | | 32 | 1 | 0 | 0 | 0 | 7 | 24 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 14 | 0 | 14 | | 2 | 0 | 0 | 0 | 4 | 8 |
| Kutorosha | 12 | 1 | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 10 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 12 | 3 | 8 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 10 |
| Shambulio | 23 | 7 | 7 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 23 |
| **Jumla** | **170** | **18** | **110** | **42** | **6** | **0** | **0** | **0** | **39** | **125** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Septemba 2022 ni 170 wote walikuwa ni wapita njia sawa na asilimia 100.

**Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia, Septemba 2022**




**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

## Kiambatanisho

### Jadweli 1.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Septemba 2022

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani | 65 | | 65 | | 29 | 29 | 6 | | 6 | 9 | 0 | 9 | 5 | 1 | 6 | 14 | 9 | 23 |
| Kazini | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 12 | | 12 | | 3 | 3 | 8 | | 8 | 3 | 0 | 3 | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **77** | | **77** | | **32** | **32** | **14** | | **14** | **12** | **0** | **12** | **11** | **1** | **12** | **14** | **9** | **23** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Jadweli 2.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Septemba 2022**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 6 | 2 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 7 | 3 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 6 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 9 | 4 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 |
| Mjini | 47 | 21 | 7 | 4 | 1 | 4 | 10 |
| Magharibi 'A' | 33 | 12 | 8 | 2 | 0 | 4 | 7 |
| Magharibi 'B' | 45 | 24 | 8 | 3 | 3 | 1 | 6 |
| Wete | 8 | 2 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **170** | **77** | **32** | **14** | **12** | **12** | **23** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Agosti na Septemba 2022**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 | Agosti 2022 | Sept 2022 |
| Kubaka | 75 | 77 | 6 | 7 | 69 | 70 | | |
| Kulawiti | 32 | 32 | | | | | 32 | 32 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 7 | 14 | 0 | 0 | 7 | 14 | | |
| Kutorosha | 3 | 12 | 0 | 1 | 3 | 11 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 12 | 12 | 4 | 3 | 5 | 8 | 3 | 1 |
| Shambulio | 2 | 23 | 2 | 7 | 0 | 7 | 0 | 9 |
| **Jumla** | **131** | **170** | **12** | **18** | **84** | **110** | **35** | **42** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Septemba 2021 na Septemba 2022**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 | Sept 2021 | Sept 2022 |
| Kubaka | 50 | 77 | 6 | 7 | 44 | 70 | | |
| Kulawiti | 14 | 32 | | | | | 14 | 32 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 3 | 14 | 0 | 0 | 3 | 14 | | |
| Kutorosha | 7 | 12 | 1 | 1 | 6 | 11 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 10 | 12 | 1 | 3 | 7 | 8 | 2 | 1 |
| Shambulio | 6 | 23 | 1 | 7 | 2 | 7 | 3 | 9 |
| **Jumla** | **90** | **170** | **9** | **18** | **62** | **110** | **19** | **42** |

**Chanzo: Makao Makuu ya Polisi –Zanzibar**

## Zingatia Maelezo

**Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia**
Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusianana maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosaya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua, 2321 Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Tovuti: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237, MMP,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136